

Taswira ya Gereza Katika Riwaya ya *Haini* ya Adam Shafi: Uhakiki wa Ki-Foucault

John Musyoka Mutua

Department of Linguistics and Languages, Machakos University, Kenya

Gerald Okioma Mogere

Email: geralgmogere@gmail.com

Department of Kiswahili, University of Nairobi, Kenya

Justus Kyalo Muusya

Email: muusyaj@yahoo.com

Department of Kiswahili, Kenyatta University, Kenya

IKISIRI

Makala hii inakusudiwa kutalii jinsi gereza ilivyotumiwa kama msingi wa kuendeleza maudhui katika riwaya ya Haini ya Shafi Adam Shafi. Aidha, inapania kudhihirisha jinsi maudhui ya jamii ya kigereza yanavyobainika kuambatana na sifa zinazotambuliwa na Michael Foucault ambaye ni mwasisi wa nadharia ya Ki-Foucault inayoongoza uhakiki huu. Aghalabu msanii wa fasihi huchota malighafi yake kutokana na jamii anamokulia pamoja na tajriba yake inayoongozwa na ubunifu wake. Pia, matukio na asasi mbalimbali za jamii hutoa mchango mkubwa katika kuendeleza maudhui katika fasihi ya Kiswahili. Gereza ni mojawapo ya asasi zinazokuwa chemichemi ya maudhui yanayoendeleza fasihi katika jamii. Maudhui ni kipengele muhimu katika kazi ya fasihi, yanapofanuliwa na kueleweka na msomaji, hapo ndipo lengo la mwandishi hukamilika. Katika msingi huu tumedhamiria kuchunguza jukumu la mfumo wa kigereza na athari zake katika jamii kwa kurejerea Haini.

Corresponding Author: Email: mutua660@yahoo.com